

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA**



# **TANGAZO**

**YAH: UANDIKISHAJI WA VIJANA WA KUJIUNGA NA JESHI LA  
KUJENGA TAIFA KWA UTARATIBU WA KUJITOLEA  
(HIARI) MWAKA 2020/2021**

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kilosa inawatangazia Wananchi wote kwamba Jeshi la Kujenga Taifa limetoa nafasi kwa Vijana wenye sifa na wanaotaka kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mwaka 2020/2021.

Mategemeo ya JKT ni kuwa na idadi kubwa ya Vijana watakaoandikishwa kutoka Vijijini zaidi ili Vijiji viweze kupata fursa ya Vijana kujifunza Uzalendo, Ukakamavu na Stadi za Kazi na baada ya kumaliza muda wao wa mafunzo kurejea makwao na kuweza kujajiri.

Kutokana na mategemeo hayo inasisitizwa kuwa Mkataba wa kujitolea katika Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ni wa miaka miwili na sio kwa lengo la kuajiriwa na JKT au kutafutiwa ajira katika Asasi, Vyombo vyta Ulinzi na Usalama na mashirika mbalimbali ya Serikali au watu binafsi. Ni muhimu ikaeleweka kuwa vijana wanaojiunga na JKT kwa kujitolea wanafanya hivyo kwa hiari yao wenyewe kwa lengo la kupata mafunzo ya kuwasaidia katika maisha yao ya baadae na kuwaandaa kulitumikia Taifa watakapohitajika.

Maombi yawasilishwe Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kabla ya tarehe **14/09/2020** usaili utafanyika ngazi ya Wilaya tarehe **16/09/2020** kuanzia saa moja (1:00) kamili Asubuhi.

**Barua za maombi zipitishwe na Watendaji wa Vijiji anakoishi muombaji zikiwa zimeambatanishwa na nakala ya vyeti vilivyoainishwa kama sifa za muombaji.**

**Sifa za waombaji ni kama ifuatavyo:-**

1. Awe Raia wa Tanzania.
2. Umri:
  - a. Kwa vijana wenge elimu ya darasa la saba umri ni kuanzia miaka 16 hadi 18.
  - b. Vijana wenge elimu ya Kidato cha Nne umri usiwe zaidi ya miaka 20.
  - c. Vijana wenge elimu ya Kidato cha Sita umri usiwe zaidi ya miaka 22.
  - d. Vijana wenge elimu ya Stashahada umri usiwe zaidi ya miaka 25.
  - e. Vijana wenge elimu ya Shahada umri usiwe zaidi ya miaka 26.
  - f. Vijana wenge elimu ya Shahada ya Uzamili umri usiwe zaidi ya miaka 30.
  - g. Vijana wenge elimu ya Shahada ya Uzamivu umri usiwe zaidi ya miaka 35.
3. Awe na afya njema, akili timamu na asiwe na alama yoyote ya michoro mwilini (Tattoo).

4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.
5. Kwa vijana waliomaliza elimu ya Sekondari, Kidato cha Nne na cha Sita wawe waliomaliza kuanzia mwaka 2017, 2018 na 2019 wenye ufaulu ufuatao:-
  - a. Wawe wamefaulu na wawe na alama (Points) zisizopungua 32.
  - b. Vijana wa Kidato cha Sita wawe na ufaulu wa daraja la kwanza hadi daraja la nne.
6. Awe na elimu ya msingi aliyehitimu darasa la saba.
7. Awe na Cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth Certificate).
8. Awe na Cheti halisi cha kumaliza shule (School Leaving Certificate).
9. Awe na Cheti halisi cha Matokeo (Original Academic Certificate/Transcript).
10. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au KMKM wala kuajiriwa na Idara nyingine Serikalini.
11. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma.
12. Asiwe amejihuisha na matumizi ya madawa ya kulevyta, bangi na yanayofanana na hayo.
13. Kwa wale wenye vipaji vyatia michezo mbalimbali na Sanaa sifa za elimu ni sawa na zilizotajwa hapo juu.

  
Yohana M. Kasitila  
**KATIBU TAWALA WILAYA  
KILOSA**

## Nakala:

**Wajumbe,  
Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya,  
Kilosa.**

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 65,  
**Kilosa.**

# Radio Jamii, Kilosa. (Litangazwe).

**Maafisa Tarafa wote,  
Wilayani – Kilosa. (Sambazeni kwa Watendaji wa Kata na  
kubandika kwenye Mbao za Matangazo).**